

# JARIDA *la* Mamlaka ya Serikali Mtandao

Toleo Na. 1 Julai - Septemba 2022

Mamlaka ya Serikali Mtandao

e-Government Authority



“  
Uadilifu na Ubunifu kwa  
Utoaji Huduma Bora kwa  
Umma  
”

Tujenge Serikali Kidijitali



ega\_tanzania



ega online tv

# **Yaliyomo ndani**

<b>Kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu.....</b>	<b>1</b>
<b>Dira.....</b>	<b>2</b>
<b>Dhamira.....</b>	<b>2</b>
<b>Kauli Mbiu.....</b>	<b>2</b>
<b>Uzingatiaji wa Sheria,Kanuni, Miongozo na Viwango.....</b>	<b>2</b>
<b>Ujenzi wa Mifumo ya TEHAMA Serikalini.....</b>	<b>3</b>
<b>Miundombinu Bora na Shirikishi ya TEHAMA.....</b>	<b>4</b>
<b>e-Mrejesho.....</b>	<b>5</b>
<b>Ifahamu Sheria ya Serikali Mtandao.....</b>	<b>6</b>
<b>e-GA Yapongezwa.....</b>	<b>7</b>
<b>Utafiti na Ubunifu Suluhihisho la Serikali Mtandao.....</b>	<b>8</b>
<b>e-GA Kuwa Kitovu cha Ubunifu Afrika Mashariki.....</b>	<b>9</b>
<b>Kamati ya USEMI Yaipongeza e-GA.....</b>	<b>9</b>
<b>MAJIIS:Mfumo Unaodziunganisha Mamlaka za Maji Nchini.....</b>	<b>10</b>
<b>Taasisi za Umma Zahimizwa Kutumia GovESB.....</b>	<b>11</b>
<b>Twaipongeza.....</b>	<b>12</b>



## KUTOKA KWA MKURUGENZI MKUU

*Mpendwa Msomaji,*

**K**aribu katika toleo la kwanza la Jarida la Mtandaoni kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA). Katika jarida hili, utasoma na kujifunza kuhusiana na kazi na huduma mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka kama vile, ujenzi wa mifumo inayoendana na mahitaji halisi ya Taasisi za Umma, utoaji wa huduma za ushauri na msaada wa kiufundi, uboreshaji wa njia za utoaji wa huduma za serikali mtandao, utengenezaji na uendeshaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA Serikalini inayosaidia kuboresha ufanisi wa uendeshaji shughuli za utoaji wa huduma kwa Umma.

Hali kadhalika, kupitia Jarida hili, utaweza kufahamu juhudhi na shughuli mbalimbali zinazofanywa na Mamlaka katika utekelezaji wa dhana ya Serikali Mtandao.

Toleo hili ni muendelezo wa matoleo mengine yanayofuata yatakayokuhabarisha juu ya jitahada za e-GA katika kukuza na kuchochea matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) nchini, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za umma na kuleta mabadiliko ya kijamii na kiuchumi.

Mwisho, nitumie fursa hii kukukaribisha tena katika kurasa hizi ili upate kuifahamu vizuri e-GA na shughuli mbalimbali inazozitekeleza

*Nakutakia usomaji mwema*

**Eng. Benedict Ndomba**

## DIRA

Kutambuliwa kuwa Taasisi inayoongoza kwa ubunifu katika kuwezesha matumizi ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma kwa umma.

## DHAMIRA

Kujenga mazingira wezeshi ya kisheria kwa ajili ya uratibu, usimamiaji na uendelezaji wa matumizi ya TEHAMA ili kuboresha utoaji wa huduma za Serikali kwa umma.

## KAULI MBIU

"Uadilifu na ubunifu kwa utoaji wa huduma bora kwa umma".

## UZINGATIAJI WA SHERIA, KANUNI, MIONGOZO NA VIWANGO

**"Hadi hivi sasa zaidi ya Taasisi za Umma 79 tumezifanya tathmini ya uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao"**

**Bi. Sultana Seiff**  
Meneja Udhibiti Wa Viwango Vya TEHAMA

Serikali imetengeneza Sheria, Kanuni, Miongozo na Viwango vya utekelezaji wa Jitihada za Serikali Mtandao ili kuhakikisha kuwa, Taasisi za Umma zinateneza jitihada hizo katika viwango na ubora unaotakiwa.

Miongozo hiyo hutoa maelekezo kwa Taasisi za Umma juu ya taratibu sahihi zinazotakiwa kufuat-

wa katika utekelezaji wa juhudini mbalimbali zinazohusu matumizi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma.

Meneja Udhibiti wa Viwango vya TEHAMA Bi. Sultana Seiff amesema, "uwepo wa miongozo hii unazisaidia Taasisi za Umma katika utekelezaji wa Serikali Mtandao na kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma zitolewazo na serikali".



"e-GA imekuwa ikifanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa Taasisi za Umma zinazingatia Sheria, Kanuni, Miongozo na Viwango vya Serikali Mtandao katika utendaji wa shughuli za Serikali", ameeleza Bi. Sultana

Baadhi ya maeneo ambayo Mamlaka imekuwa ikiyafanya ukaguzi katika Taasisi za Umma ni pamoja na uzingatiwaji wa Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, uzingatiwaji wa viwango na miongozo katika uhifadhi data na tathmini ya mapitio ya mifumo ya TEHAMA.

Aidha, Bi. Sultana amesema, "Mamlaka imekuwa ikifanya vikao mbalimbali vya kiufundi na Taasisi za Umma kwa lengo la kutoa msaada, ushauri na elimu juu ya uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Serikali Mtandao". Vilevile, Taasisi za Umma zimekuwa zikiwasilisha nyaraka mbalimbali za TEHAMA kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao, kwa ajili ya mapitio na kupata ushauri wa kiufundi na mabore-

sho. Hadi sasa takribani nyaraka 263 kutoka Taasisi sisi mbalimbali za umma zimefanyiwa mapitio.

Mwisho, Bi. Sultana amezitaka Taasisi zote za Umma kutekeleza jitihada za Serikali Mtandao katika viwango na ubora unaotakiwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo ili kujenga mifumo yenye tija.

“

**Ni wajibu  
wa kila  
Taasisi ya  
Umma  
kuhakikisha  
inazingatia  
Viwango na  
Miongozo  
ya Serikali  
Mtandao  
katika Utenda-  
ji kazi wao**

”

## UJENZI WA MIFUMO YA TEHAMA SERIKALINI

**M**amlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) yenye jukumu la Kuratibu, Kusimamia na Kukuza jitihada za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma, imeshirikiana na Taasisi za Umma kuleta mapinduzi katika matumizi ya Mifumo ya TEHAMA Serikalini. Matumizi hayo yanalenga kuleta ufanisi na kurahisisha utendaji kazi.

e-GA kwa kushirikiana na Taasi si za Umma, imesanifu na kutengenezwa Mifumo mbalimbali ikiwa ni pamoja na *Mfumo wa Ukusanyaji wa Malipo ya Serikali Kielektroni (GePG)*, *Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office)*, *Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwateru (HCMIS)*, *Mfumo wa Pamoja wa Uondoshaji wa Shehena Maeneo ya Forodha (TeSWS)*, *Mfumo wa Usimamizi wa Shughuli za Mamlaka ya Maji (MAJIIS)*.

Mifumo mingine ambayo imesanifiwa na kutengenezwa na Mamlaka kwa lengo la kuongeza ufanisi na kurahisisha utendaji kazi ni *Mfumo wa Baruapepe Serikalini (GMS)*, *Mfumo wa Huduma za Serikali kupitia simu za Mkononi (Government Mobile Platform - mGov)* \*152\*00# (Menyu) & 15200 (SMS), *Mfumo wa Vibali (e-Vibali)* na *Mfumo wa Mikutano kwa Njia ya Mtandao (e-Mikutano)*.

Kaimu Meneja wa Huduma za Ushauri na Uelekezi Bi. Joan Valentine amesema kuwa kazi hizi zinafanya ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sheria ya Serikali Mtandao ambayo inaitaka e-GA kuwezesha Taasisi za Umma kupata miundombinu na mifumo ya TEHAMA ya pamoja ili kupunguza gharama za uendeshaji Serikalini.




Bi. Joan Valentine  
Kaimu Meneja wa Huduma za Ushauri na Uelekezi

*Serikali kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao imeten-geneza mifumo wa Ubadilishanaji taarifa unaojulikana kama Government Enterprise Service Bus - GovESB ikiwa ni jitihada za kuhakikisha Mifumo inabadilishana taarifa*

”

Bi. Joan Valentine  
Kaimu Meneja wa Huduma za Ushauri na Uelekezi



# MIUNDOMBINU BORA NA SHIRIKISHI YA TEHAMA NI MUHIMU KATIKA KUBORESHA UTOAJI WA HUDUMA KWA UMMA



**Sheria ya Serikali Mtandao inazitaka na kuelekeza kuwa taasisi za umma zinazohusika na ujenzi wa miundombinu ya serikali kama vile barabara, reli na majengo kuhakikisha kuwa yanawekewa mazingira wezeshi kwa ajili ya kupitisha miundombinu ya TEHAMA kuanzia wakati wa kuandaa michoro ya ujenzi wa miundombinu hiyo.**

**Eng. Kulwa Kapama  
Meneja Usimamizi wa Mtandao  
wa Mawasiliano**

**S**erikali inaweka Miundombinu salama ya TEHAMA inayoziwesha Taasisi za Umma kushirikiana katika matumizi ya rasilimali za TEHAMA ili kuondoa urudufu, kupunguza gharama na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma, pamoja na kuhakikisha usalama wa mawasiliano.

Miundombinu iliyopo ni pamoja na Mkongo wa Taifa (NICTBB), Mtandao wa Serikali (GovNet), Vi-

Hali kadhalika, mamlaka imetua huduma ya Masafa ya Internet "bandwidth" kwa Taasisi za Umma 554 ili kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii.

Hayo yameelezwa na Meneja Usimamizi wa Mtandao wa Mawasiliano Bw. Kulwa Kapama alipofanya mahojiano na mwandishi wetu ofisini kwake jijini Dar es Salaam.

Bw. Kapama amesema kuwa, Sheria ya Serikali Mtandao inazitaka na Taasisikuzielekeza Taasisi za Umma zinazohusika na ujenzi wa Miundombinu ya Serikali kama vile barabara, reli na majengo kuhakikisha kuwa zinawekewa mazingira wezeshi, kwa ajili ya kupitisha Miundombinu ya TEHAMA kuanzia wakati wa kuandaa michoro ya ujenzi wa miundombinu hiyo.

Bw. Kapama ameongeza kuwa, Miundombinu ya TEHAMA Serikali ni imesaidia kuboresha mawasiliano katika Taasisi za Umma na kurahisisha upatikanaji wa huduma mtandao zinazotolewa na Taasisi hizo.

Aidha, Bw. Kapama amesisitiza kuwa, kupitia Miundombinu hiyo, Taasisi zote za Umma zinaunganishwa kwenye mtandao mmoja wa mawasiliano ambao ni salama na wenyewe gharama nafuu ili kuziwesha Taasisi hizo kuwa na mawasiliano ya kielektroni.

Hadi hivi sasa, zaidi ya Taasisi 394 kutoka Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa, hospitali, Taasisi za Elimu ya Juu, Mahakama na Mamlaka za Maji zimeunganishwa katika mtandao wa Mawasiliano (GovNet).

“  
**Taasisi zote za umma zimeunganishwa kwenye Mtandao wa Serikali (Government Network) hii inatusaidia kujua maeneo ambayo kuna matatizo na kuweza kupata utatuzi wa haraka**  
“

# e-MREJESHO NI SULUHISHO LA KERO ZA WANANCHI

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kuititia Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imetengeneza Mfumo wa kidigitali ujulikanao kama *e-Mrejesho*, unaomuwezesha mwananchi kuwasilisha malalamiko, kero, maoni, mapendekezo, au maulizo moja kwa moja kwenye Taasisi /Wizara husika sambamba na kufuutilia utekelezaji wake.

Mfumo huo wa kidigitali una lengo la kumsaidia mwananchi kupunguza gharama pamoja na kuokoa muda wa kutembea umbali mrefu ili kuwasilisha maoni, mapendekezo au kufuutilia malalamiko yake.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Jenista Mhagama (Mb) amesema kuwa, Mfumo wa e-Mrejesho ni suluhisho kwa wananchi kwani unamuwezesha mwananchi kuwasiliana na serikali moja kwa moja na kuwasilisha maoni yake kuititia simu ya kiganjani.

Aidha, Waziri Mhagama ameelia kuwa, Mfumo wa e-Mrejesho umeongeza ufanisi wa utendaji kazi serikalini katika utoaji wa huduma kwa wakati na kwa ubora, kwari watumishi wa umma wanaweza kujibu malalamiko au maoni ya wananchi wengi kwa muda mfupi kuititia mfumo huo.

Waziri Mhagama amesisitiza kuwa, kutohana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia Mfumo wa e-Mrejesho umekuwa ni fursa nzuri kwa wananchi kuwasiliana na serikali kwa urahisi na haraka zaidi hivyo amewata wananchi kutoogopa kuutumia Mfumo huo.



**“Mfumo wa e-Mrejesho utasidia kuboresha na kuimarisha mahusiano mazuri kati ya wananchi na serikali kwani, mfumo huu utasidia kutatua changamoto za wananchi kwa wakati, pia utasidia kujua je, wananchi wanasema nini kuhusu serikali, Je huduma zipo vizuri?”**

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Mhandisi Benedict Ndomba amesema kuwa, Mfumo wa e-Mrejesho ni salama na umezingatia usiri mkubwa wa taarifa kwani mwananchi anapowasilisha maoni au malalamiko yake, Mfumo unampa nafasi ya kuchagua kujulikana au kutojulikana kwa kuandika au kutoandika taarifa zake binafsi.

*“Napenda kuwahakikisha kuwa, Mfumo huu ni salama kutumia kwani unampa nafasi mwananchi ya kuchagua kujulikana kwa kuandika majina yake na namba za simu na kama hatopenda basi ataacha wazi”*, amesisitiza Mhandisi Ndomba.

Aidha, Mkurugenzi amesema kuwa, Mfumo huu wa e-Mrejesho

unaziunganisha Taasisi zote za Serikali hivyo, Taasisi kwa Taasisi zinaweza kubadilishana taarifa za malalamiko au maoni yanayotolewa na wananchi na pia serikali inaweza kupata takwimu za malalamiko hayo.

Mhandisi. Ndomba ametoa wito kwa wananchi wote kuupenda na kuutumia Mfumo huo wa kidigitali ili kuongeza ufani si katika Taasisi za Umma kwenye utoaji wa huduma kwa jamii sambamba na kuunga mkono Jitihada za Serikali Mtandao.

Mfumo wa emrejesho unapatikana katika tovuti ya [www.emrejesho.go.tz](http://www.emrejesho.go.tz), au kwa kupakua ‘application’ ya eMrejesho kwa kutumia simu janja au kupiga namba \*152\*00# kisha chagua namba 9, kisha chagua 2 na kisha fuata maelekezo



**“Mfumo huu umekuwa msaada mkubwa kwa wananchi hasa katika kupata mrejesho na majawabu ya matatizo yao”**

Mhandisi Benedict Ndomba  
Mkurugenzi Mkuu eGA

## IFAHAMU SHERIA YA SERIKALI MTANDAO

Sheria ya Serikali Mtandao **Na. 10 ya mwaka 2019** inaelekeza matumizi sahihi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma. Sheria hii ndiyo imeunda Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na kuainisha majukumu yanayoiongoza Mam-laka katika utekelezaji wa Jitiha-da za Serikali Mtandao nchini.

Majukumu hayo ni pamoja na kura-tibu, kusimamia na kukuza jiti-hada za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza utekelezaji wa Sera, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma.

Sheria ya Serikali Mtandao, ime-ipa Mamlaka jukumu la kutoa ushauri wa namna ya utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya TEHA-MA pamoja na kuruhusu kuen-delea kwa Miradi hiyo, ikiwa ni pamoja na kuzitaka Taasisi husi-ka kutoa taarifa za utekelezaji mara kwa mara pamoja na taarifa ya mwisho baada ya kukamilika kwa Miradi hiyo.

Aidha, Mamlala inalo jukumu la kutoa katazo la kutoendelea kwa Miradi wowote wa TEHAMA endapo utabainika kutokuwa na tija kwa Taifa.TaasisiTaasisi

Vilevile, Sheria inaelekeza kunapokuwa na ujenzi wa Mi-undombinu yeyote ya Sserikali kama vile barabara, reli, majengo lazima kuwe na utayari wa kuwe-ka miundombinu na mifumo ya TEHAMA chini ya usimamizi wa wataalamu wa ndani, ili kuonge-za tija katika utendaji kazi.

Hayo yameelezwu na Meneja wa Huduma za Sheria Mamlaka ya Serikali Mtandao, ACP Raphael Rutaihiwa wakati wa mahojiano na mwandishi wetu jijini Dodoma.

Rutaihiwa amesema kuwa, uwe-

po wa sheria ya Serikali Mtandao na kanuni zake unasaidia kuwezesha matumizi sahihi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma yanayopelekea kuboresha kwa utendaji kazi na kutoa huduma bora zinazopatika-na kwa urahisi na haraka, na hivyo kuwa na Serikali ya Kidigitali iliyo imara na endelevu.



*"Sheria ya Serikali Mtandao ina-izitaka na kuzielekeza Taasisi za Umma zinazohusika na ujenzi wa Miundombinu ya Serikali kama vile Barabara, Reli na Majengo, kuhakikisha yanawekewa mazingira wezeshi kwa ajili ya kupitisha Miundombinu ya TEHAMA kuanzia wakati wa kuandaa michoro ya ujenzi wa miundombinu hiyo"*

amesema Rutaihiwa na kuongeza kuwa,

*"Sheria ya Serikali Mtandao inazi-taka Taasisi za Umma kuwasilisha mapendekezo na nyaraka zote zin-azohusu miradi ya TEHAMA kab-la ya kuanza utekelezaji, kwa ajili ya kuhakikiwa na kupitishwa na Mamlaka na baadae kuwasilisha taarifa za maendeleo ya utekelezaji pamoja na taarifa ya mwisho baada ya kukamilika kwa mradi husika"*

ACP Rutaihiwa amesema, uzingati-waji wa Sheria ya Serikali Mtandao na Kanuni zake, utasaidia kuwa na matumizi sahihi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma hivyo kuwa na utendaji kazi wenye tija na ufanisi na utoaji wa huduma zinazopatikana kwa urahisi na kwa gharama nafuu.

**Sheria hii ni kama muongozo wa namna gani Taasi-si za Umma zinatakiwa kufanya kwenye eneo la TEHAMA.Nazisi-hi Taasisi za umma kuisoma Sheria hii na kuilewa ili TEHAMA iweze kulete tija kwenye Taasisi zao**

**ACP Raphael Rutaihiwa**

**Meneja wa Huduma za Sheria**

## e-GA YAPONGEZWA KWA USIMAMIZI WA MATUMIZI YA TEHEMA SERIKALINI

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Kundo A. Mathew (Mb) ameipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kazi nzuri ya kusimamia na kuhakikisha Taasisi za Umma zinakuwa na matumizi sahihi ya TEHAMA..


Pongezi hizo alizitoa wakati wa kongamano la miaka 60 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), na miaka 10 ya Ndaki ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (CoICT) lililofanyika Septemba 23, 2022 katika viwanja vya ndaki hiyo vilivyopo Kijitonyama jijini Dar es Salaam..



**"Nachukua fursa hii kuipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kazi nzuri inayoifanya ya kuziunganisha Taasisi zote za Umma, na kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi na salama ya Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA Serikalini. Pia, nitumie fursa hii kuiomba e-GA kuendelea na usimamizi wa Taasisi za Umma ambazo bado ziponyuma kwenye matumizi ya TEHAMA"**

**Mhe. Kundo Mathew**  
Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

Aidha, Rais wa Ndaki ya TEHAMA ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Prof. Joel S. Mtebe ameishukuru e-GA kwa ushirikiano mzuri inayoipatia ndaki hiyo hususani kwenye masuala ya TEHAMA katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao.



"Mamlaka imekua msaada mkubwa sana kwetu kwakuwa, inatoa ushauri na msaada wa kiufundi katika masuala mbalimbali ya TEHAMA kwa wakati, kila mara inapohitajika", amesema Prof. Mtebe.

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ilipata tuze ya udhamini ya kongamano hilo iliyopokelewa na Mkurugenzi wa Miundombinu na Uendeshaji wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Bw. Benjamin Dotto..

“

Tunaishukuru sana Mamlaka ya Serikali Mtandao eGA kwa kuwa nasi chuo kikuu cha Dar Es Salaam hasa hapa ndaki ya TEHAMA,tunasa idiana katika maeneo mbalimbali,tunaomba ushirikiano huu uendelee ili kuhakikisha TEHAMA inakua kiungo muhimu katika kujenga uchumi wa nchi yetu

”

Prof. Joel Mtebe  
*Rasi Ndaki ya TEHAMA UDSM*



## UTAFITI NA UBUNIFU SULUHISHO LA SERIKALI MTANDAO

Wanafunzi wanaofanya mafunzo kwa vitendo katika fani ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), wameaswa kufanya utafiti na kuwa wabunifu katika masuala ya Serikali Mtandao ili kutengeneza mifumo inayoweza kutatua changamoto zilizopo katika jamii.



Kauli hiyo imetolewa na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deogratius Ndejemb (Mb), wakati akifunga programu ya nne ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, kwenye Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji Serikali Mtandao cha Mamlaka ya Serikali Mtandao (GovRIDC) Septemba 12, mwaka huu jijini Dodoma.

Mhe. Ndejemb aliongeza kuwa, muda wa wiki nane zilizopangwa kwa vijana hao zimekuwa za mafanikio makubwa baada ya kuona kazi nzuri ambazo zimefanyika na kuamini kuwa ujuzi walioupata vijana hao utasaidia katika kukuza uchumi wa nchi.

Naye, Kaimu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Bw. Cosmas Ngangaji amesema kuwa, hivi sasa dunia ipo kwenye kipindi cha nne cha mapinduzi ya viwanda ambacho

TEHAMA ni kipaumbele katika kufikia mapinduzi hayo, na kuwataka wanafunzi hao kutumia fursa waliyoipata kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa umma kwa njia ya TEHAMA.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Mhandisi. Benedict Ndomba, amesema kuwa ofisi yake inachukua vijana wanaofanya vizuri katika vyuo mbalimbali vya elimu ya juu, kwa lengo la kuwaongeza uwezo na ujuzi zaidi ili kuwa wabunifu katika masuala yanayohusu serikali mtandao.

*"Vijana hawa wamekuwa wakinu-faika sana na uwepo wa kituo hiki kwa kuwa wote waliopita katika kituo hiki wameajiriwa aidha na serikali au sekta binafsi"* alisisitiza Mhandisi Ndomba.

17:14



Vijana hawa wana-saidia katika kuibua changamoto zinazoi-kabili jamii na kuzipatia majibu. Mfano kupitia vijana hawa tumeweza kutengeneza mifumo kama e-Mrejesho, e-Miku-tano na e-dodoso

Mhandisi Benedict Ndomba  
Mkurugenzi Mkuu eGA



### eMrejesho

Mfumo wa Kutuma, Kupokea na Kufuatilia Malalamiko, Mapendekezo, Maulizo na Pongezi

### #IAMBIE\_SERIKALI



## e-GA KUWA KITOVU CHA UBUNIFU AFRIKA MASHARIKI

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Jenista Mhagama (Mb), ameitaka Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kuwa kioo na kitovu cha ubunifu, usanifu na utengenезaji wa mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Mh. Jenista ametoa kauli hiyo Septemba 09, mwaka huu katika ofisi za Bunge jijini Dodoma, mara baada ya Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi. Benedict Ndomba kuwasilisha mada kuhusu Usalama wa Serikali Mtandao kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, iliyolenga kuwajengea uwezo viongozi hao kuhusu usalama wa mitandao.



"Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan inatambua mchango wa e-GA katika kuboresha utendaji kazi Serikalini, lakini tunatakiwa kuwa wabunifu zaidi ili Mifumo ya TEHAMA inayotengenezwa na e-GA iweze kuuzwa katika nchi jirani za Afrika ya Mashariki"

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mhe. Daniel Sillo (Mb) ameileza kuridhishwa na utendaji kazi wa e-GA na kuitaka kuen-deleza jitihada za ubunifu na kuhakisha usalama wa mifumo ya TEHAMA unakuwepo ili kudhibiti upotevu wa fedha za Serikali hasa katika Halmashauri.

Aidha, wajumbe wa Kamati hiyo wameipongeza e-GA kwa kutekeleza vema majukumu yake na kuitaka kutoa elimu kuhusu usalama wa mitandao kwa wananchi ili kuwajengea uelewa na kuweza kulinda taarifa zao katika mitandao.

### KAMATI YA USEMI YAIPONGEZA e-GA

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa (USE-MI), imeipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa kuendelea kusimamia na kubuni Mifumo tumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), inayorahisisha utendaji kazi wa serikali katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Pongezi hizo zimetolewa Septemba 9, Mwaka huu na Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Abdallah Chaur-embo katika Ofisi za Bunge Jijini Dodoma, mara baada ya Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi. Benedict Ndomba kuwasilisha mada kuhusu Usalama wa Serikali Mtandao, ili kuwajengea uwezo viongozi hao kuhusu usalama wa mitandao.

Mhe. Chaurembo alisema ameridhishwa na utendaji kazi wa e-GA ikiwa ni pamoja na jitihada za kubuni na kutengeneza mfumo wa e-Mrejesho ambao unasaidia wananchi kuwasilisha maoni au malalamiko yao pamoja na kufuatilia utekelezaji wake ili kupata majibu sahihi kutoka katika Taasisi husika.

Kwa upande wake Mjumbe wa Kamati ya USE-MI Mhe. Dkt.Thea Ntala ameipongeza e-GA kwa ubunifu wa Mifumo mbalimbali ya serikali, alitaja mionganii mwa Mifumo hiyo ni pamoja na *Mfumo wa Ukusanyaji Malipo ya Serikali kwa Njia ya Kielektroni (GePG)*.



Mhe. Abdallah Chaurembo  
Mwenyekiti wa Kamati

Aidha, Mhe. Dkt. Ntala alieleza kuwa, Mfumo huo umeisaidia serikali kuku-sanya fedha kwa ufanisi mkubwa na kupunguza ubadhifuru na upotevu wa fedha za umma. Pia, Mfumo wa Pamoja wa Utoaji Ankara za Maji (Maji Intergrated and Unified Billing System-MAJIIS) ili kurahisisha uendeshaji, usimamizi na kuongeza mapato ya Mamlaka za Maji na Serikali kwa ujumla.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Jenista Mhagama (Mb) ameitaka e-GA kuongeza juhudii zaidi katika kubuni na kutengeneza Mifumo ya TEHAMA inayotatua changamoto mbalimbali zilizopo katika mazingira yetu na jamii kwa ujumla.

Vile vile, Mkurugenzi Mkuu wa e-GA Mhandisi, Benedict Ndomba amewasisitiza wabunge na wananchi kwa ujumla kuwa makini, ili kuepuka udukuzi wa taarifa zao pindi wanapotumia vifaa vya kielektroni kama vile vishikwambi, kompyuta na simu za mkononi ikiwa ni pamoja na kutofungua viunganishi (links) wanazotumiwa bila ya kuzielewa vizuri ili kujiepusha kudukuliwa kwa taarifa zao.

## MAJIIS: MFUMO UNAOZIUNGANISHA MAMLAKA ZA MAJI NCHINI

Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kushirikiana na Wizara ya Maji imesanifu na kutengeneza *Mfumo wa Pamoja wa Utoaji Ankara za Maji (Maji Intergrated and Unified Billing System-MAJIIS)* kwa lengo la kurahisisha uendeshaji, usimamizi na udhibiti wa mapato ya Mamlaka za Maji na Bodi za maji za Mabonde Tanzania.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Mhandisi, Benedict Ndomba amesema kuwa, awali taasisi nyingi za maji hazikuwa na mifumo inayorahisisha utendaji kazi na baadhi ya taasisi zilikuwa na mifumo ambayo haikuwasiliana.

Hali hiyo ilipelekea upatikaji wa taarifa za wateja pamoja na makusanyo kuchukua muda mrefu na wakati mwengine taarifa hizo hazikuwa sahihi na hivyo Wizara ya Maji kwa kushirikiana na Mamlaka ikatengeneza mifumo wa MAJIIS ili kutatua chan-gamoto hizo.

"Mfumo huu ni muhimu kwa taasisi za maji kwani umerahisisha utoaji huduma na ukusanyaji mapato kufanyika kwa

ufanisi zaidi pia, utoaji wa huduma kwa umma umerahisisha kwa kuwezesha ulipaji wa ankara za maji kufanyika kwa wakati na mahali popote, kwa kutumia vitumi vya kielektroni kama kompyuta na simu za mkononi" amesema Mhandisi Ndomba.

Aidha, Mhandisi Ndomba amezihimiza Mamlaka za Maji pamoja na Bodi za Maji za Mabonde amba zo bado hazijaunganishwa kwenye mfumo huo kufanya jitihada za makusudi za kuunganishwa katika mfumo ili kuondoa kero mbalimbali kwa wananchi.

Akifafanua kuhusu mfumo huo Meneja wa Kitengo cha Huduma za Serikali Kupitia Simu za Mkononi wa Mamlaka Bw. Abdallah Samizi amesema kuwa, mfumo huo umeleta ufanisi, uwazi, na umesaidia kupunguza mianya ya rushwa kwa kuondoa ulazima wa mteja na mtoa huduma wa taasisi ya maji kukutana ana kwa na ili kupata huduma.

*"Kwa sasa mteja anaweza kujuhudumia mwenyewe kupitia simu yake ya mkononi kwa kupiga namba \*152\*00#, atachagua namba 6 Maji, kisha 1 Huduma za pamoja za maji ambapo atakutana na orodha inayooonesha huduma mbalimbali za maji na atachagua kadiri ya hitaji lake"* amesema Bwa.Samizi.

Bwana Samizi amefanua kuwa MAJIIS ni mfumo shirikishi na ume-tengenezwa kwa lengo la kuziwezesha Mamlaka za Maji kuendesha shughuli zao katika mfumo mmoja.

Aidha, ameongea kuwa mfumo huo unaruhusu Maafisa mbalimbali wa Taasisi pamoja na Afisa Masuuli pamoja na Maafisa wengine wa Taasisi kufuatiatarifa za uso-maji wa dira za wateja zinazokusanywa na watenda-ji katika ngazi mbalimbali, vilevile unatoa uwezo wa kuhakiki taarifa hizo kabla ya ankara ya maji kum-fikia mteja.

*"Mfumo wa MAJIIS unasaidia kufanya tathmini ya matumizi ya maji ya mteja katika vipindi tofauti vya matumizi na kumuhakikisha mteja kupata ankara ya maji sahihi kutokana na matumizi yake"*

**Bw. Abdallah Samizi**  
Meneja wa Kitengo cha Huduma za Serikali Kupitia Simu za Mkononi wa Mamlaka



## TAASISI ZA UMMA ZAHIMIZWA KUTUMIA GovESB

Kifungu cha 48 (2) cha Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019, kinaitaka Mamlaka ya Serikali Mtandao kuanzisha na kuendesha Mfumo wa unaowezesha Mifumo ya TEHAMA Serikalini kuwasiliana na kubadilishana taarifa.

Katika utekelezaji wa matakwa ya kisheria, e-GA imesanifu, kutengeneza na kusimamia mfumo unaowezesha Mifumo ya serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa unaojulikana kama *Government Enterprise Service Bus (GovESB)*.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Mhandisi. Benedict Ndomba amesema kuwa, awali Taasisi za Umma zilitengeneza mifumo mbalimbali ambayo haikuwa na uwezo wa kuwasiliana na kubadilishana taarifa. Mhandisi Ndomba ameeleza kuwa, e-GA imetengeneza Mfumo wa GovESB ili kuwezesha mifumo hiyo kubadilishana taarifa kwa wakati ili kupunguza adha kwa wananchi katika upatikanaji wa huduma.

**“Mfumo huu unarahisisha utoaji wa huduma kwa mwananchi kwa kuwa taarifa zote zinapatikana katika dirisha moja na zinavutwa kutoka Taasisi moja hadi nyingine kutokana na makubaliano ya Taasisi hizo kulingana na huduma na mahitaji” amesema Mhandisi. Ndomba.**

Baadhi ya Taasisi ambazo zimeunganishwa katika Mfumo huu ni pamoja na *Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)*, *Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA)*, *Mahakama, Mamlaka za Bima, Tume ya Vyuo Vi-kuu (TCU) na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali*.

Aidha, Mhandisi. Ndomba ametoa wito kwa Taasisi za Umma kuwasilisha makubaliano yao na Taasisi wanazotaka kubadilishana taarifa ili Mamlaka iwasaidie kuunganisha Mifumo yao ili kupata taarifa kwa urahisi pamoja na kuo-ko muda na garama.

Naye, Meneja wa Usimamizi wa Ujenzi wa Mifumo ya TEHAMA e-GA Bw. Fratern Hassan amesema kuwa GovESB inalenga kutatua changamoto za ubadilishanaji wa taarifa kuto-ka mfumo moja hadi mwingine serikalini.



### Mfumo unaowezesha Mifumo ya TEHAMA Serikalini kubadilishana taarifa

“  
Ni wajibu wa Taasisi za Umma kuhakikisha mifumo yenu imeunganishwa kwenye mfumo huu wa GovESB ili kuondokana na changamoto ya mifumo kutokubadilishana taarifa ambalo limekuwepo kwa muda mrefu  
”

Mhandisi Benedict Ndomba  
Mkurugenzi Mkuu eGA

# TWAIPONGEZA



**“Naipongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kutengeneza Mfumo wa Kielekitroniki unaojulikanakama OAGMIS pia niwaombe sana wale wanaopaswa kuutumia wautumie vema kwa faida ya Taifa letu”**

Mhe. Samia Suluhu Hassan  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

[f ega\\_tanzania](#) [eGA online tv](#)



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Kassim Majaliwa** akimkabidhi cheti cha udhamini wa Kongamano Mkurugenzi wa Usimamizi wa Huduma za TEHAMA **Bw. Ricco Boma** wakati wa Kongamano la Sita (6) la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Iilihofanyika tarehe 19 Septemba 2022 jijini Dodoma.

[f ega\\_tanzania](#) [eGA online tv](#)



Naibu Waziri wa Wizara ya Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari **Mhe. Kundo A. Mathew (Mb)** akimkabidhi tuzo ya udhamini Mkurugenzi wa Miundombinu na Uwezeshaji eGA **Bw. Benjamin Dotto** wakati wa Kongamano la Miaka 60 ya Chuo kikuu cha Dar Es Salaam na Miaka 10 ya ndaki ya TEHAMA (CoCT) Iilihofanyika Septemba 23 mwaka huu jijini Dar Es Salaam.

[f ega\\_tanzania](#) [eGA online tv](#)

**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano cha  
Mamlaka ya Serikali Mtandao kikiongozwa na bodi ya  
wahariri.**

Mwenyekiti : *Eng. Benedict Ndomba*

Mhariri Mkuu : *Subira Kaswaga*

Mhariri Msaidizi : *Rainer Budodi*

Waandishi : *Queenter Mawinda*  
*Catherine Peter*

Msanifu wa picha : *Edger Msamba*

Mpiga picha : *Mussa Enock*

*"Karibu tujenge Serikali kidijitali"*

**Mamlaka ya Serikali Mtandao  
S.L.P 2833 Dodoma,  
Mtaa wa Mtandao,**

**MTUMBA**

Tovuti: [www.ega.go.tz](http://www.ega.go.tz)  
Barua pepe: [info@ega.go.tz](mailto:info@ega.go.tz)